ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

# TAARIFA KWA UMMA

## MAKUSANYO YA KODI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Zanzibar, 01 Julai, 2024:**

### 1. MAKUSANYO YA JULAI 2023 – JUNI 2024

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), tunautaarifu Umma kwamba katika Mwaka wa Fedha, 2023/2024, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa Kushirikiana na Walipakodi wote wa Zanzibar, **IMEFANIKIWA** kukusanya Jumla ya **Tshs. 718.760 bilioni**, kati ya lengo la kukusanya **Tshs. 675.601 bilioni**, ambao ni **UFANISI** wa **asilimia 106.39** ya lengo la Makusanyo ya Kodi tarajiwa.

Kipekee, **TUNAWASHUKURU** sana **Walipakodi** wote na **Wananchi** wa Zanzibar kwa **UWAJIBIKAJI** wa Ulipaji Kodi wa Hiari kwa kipindi cha mwaka mzima kilichopelekea kufikia Mafanikio haya. ZRA, **INAWAPONGEZA** sana Walipakodi wote kwa Kutimiza Wajibu wenu wa Kiraia wa Kulipa Kodi kwa Hiari na kwa **USHIRIKIANO** mkubwa mnaoutoa kwa ZRA.

Kwa mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Makusanyo halisi ya kodi ya **Tshs. 718.760 bilioni**, **YAMEONGEZEKA** kwa **asilimia 27.01**, ambacho ni kiasi cha **Tshs 152.869 bilioni**, ukilinganisha na mapato halisi ya mwaka wa Fedha uliopita wa 2022/2023, ambayo yalikuwa **ni Tshs 565.890 bilioni**. Sambamba na hilo, kwa mara ya kwanza, ZRA kwa kushirikiana na Walipakodi, **IMEFANIKIWA** kuweka **REKODI** ya **KUVUKA** lengo na Kuongeza makusanyo kwa kila mwezi ndani ya miezi yote kumi na mbili ya mwaka wa Fedha 2023/2024, na kufikia **UFANISI** na **UKUAJI** wa **asilimia 106.39** na **asilimia 27.01**, mutawalia. Jedwali Nam. 1 linatoa ufafanuzi zaidi.

***Jedwali Nam. 1: Makusanyo ya Mapato kwa Mwezi Mwaka 2023/2024***

| | 2022/2023 | 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwezi** | **Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)** | **Makisio (Tshs. Billioni)** | **Makusanyo Halisi (Tshs. Bilioni)** | **Ufanisi** | **Ongezeko (Tshs. Billion)** | **Ukuaji** |
| Julai | 37.674 | 42.437 | 42.897 | 101.08% | 5.223 | 13.86% |
| Agosti | 46.248 | 55.616 | 57.238 | 102.92% | 10.990 | 23.76% |
| Septemba | 47.870 | 59.002 | 61.694 | 104.56% | 13.824 | 28.88% |
| Octoba | 48.682 | 58.120 | 61.201 | 105.30% | 12.519 | 25.72% |
| Novemba | 55.931 | 60.888 | 65.222 | 107.12% | 9.289 | 16.61% |
| Disemba | 49.685 | 59.318 | 63.514 | 107.07% | 13.828 | 27.83% |
| Januari | 53.245 | 66.568 | 70.181 | 105.43% | 16.936 | 31.81% |
| Februari | 56.766 | 70.770 | 72.925 | 103.04% | 16.159 | 28.47% |
| Machi | 53.178 | 63.488 | 64.610 | 101.77% | 11.431 | 21.50% |
| April | 43,735 | 51,992 | 60,080 | 115.56% | 16,344 | 37.37% |
| Mei | 35,357 | 42,212 | 50,299 | 119.16% | 14,942 | 42.26% |
| June | 37,514 | 45,187 | 48,894 | 108.21% | 11,380 | 30.34% |
| **Jumla** | **565,890** | **675.601** | **718,760** | **106.39%** | **152,869** | **27.01%** |

**Chanzo:** Mamlaka ya Mapato Zanzibar 2024

## 2. SABABU ZA KUFANYA VIZURI:

Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya Kodi kwa **asilimia 106.39**, na ongezeko la kodi kwa **Tshs 152.869 bilioni**, pamoja na mambo mengine umesababishwa na:

I. **KUIMARIKA** kwa **Mahusiano** na **Ushirikiano** kati ya ZRA na Wafanyabiashara wote wa Zanzibar kulikopelekea **KUONGEZEKA** kwa ulipaji kodi wa hiari .

II. **UWEKEZAJI** mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na **KUIMARIKA** kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar na ongezeko la watalii linalotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

III. **KUIMARIKA** na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na sera na uongozi mzuri wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilizoimarisha mazingira ya biashara kwa pande zote mbili za Muungano.

IV. **KUONGEZEKA** wigo wa Walipakodi kwa kusajili Walipakodi wapya **6,982** wa makundi mbali mbali na kuwasajili Walipakodi **2,876** katika mfumo mpya wa ZIDRAS.

V. **KUONGEZEKA** kwa **UFANISI** wa ZRA katika kufanya kazi kwa uweledi, Kuimarisha huduma bora za kodi katika ofisi za Mikoa ya kikodi na Vituo vya kutolea huduma za kodi kwa Unguja na Pemba, Kuongezeka kwa utoaji wa elimu ya kodi na Kuimarisha matumizi sahihi ya mifumo ya ukusanyaji kodi ya VFMS na ZIDRAS.

VI. **KUSIMAMIA UADILIFU** kwa Watumishi wa ZRA ambapo watumishi wote walijaza fomu ya **TAMKO** la mali na madeni sambamba na kutokuwepo kwa **KESI** yoyote ya uvunjifu wa maadili iliyotolewa taarifa kwa Mamlaka pamoja na kuendelea kufuatilia nyendo za watumishi katika kutoa huduma nzuri kwa walipakodi.

VII. **KUWAFIKIA** na **KUWASILIKILIZA** Walipakodi moja kwa moja katika shughuli zao za kiuchumi, kupitia kituo cha Mawasiliano kwa Walipakodi cha ZRA (ZRA Contact Center) na Programu ya kupokea Maoni ya Wafanyabiashara kwa njia ya mtandao (ZRAFunguka App).

VIII. **KUIMARIKA** kwa ushirikiano na Taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Kamisheni ya Utalii, Ofisi za Uhamiaji pamoja na taasisi zote za Serikali.

## 3. MIKAKATI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025:

Katika kuimarisha Ukusanyaji wa Mapato ya Kodi kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, ZRA, itaendelea kutekeleza yafuatayo:

I. **KUENDELEA** kuimarisha **MAHUSIANO** mazuri na **USHIRIKIANO** na walipakodi wote ikiwemo kusaidia kurahisisha biashara zao kisheria (Trade Facilitation) pamoja na kuimarisha matumizi sahihi ya Mifumo katika usimamizi wa kodi ikiwemo matumizi ya mfumo wa **RISITI ZA KIELEKTRONIKI (VFMS)**, na matumizi ya mfumo wa **ZIDRAS**.

II. **KUTATUA** changamoto za Wafanyabiashara na Migogoro ya Kikodi kwa wakati, ikiwemo kuweka mazingira ya usimamizi wa sheria za kodi yatakayoondoa changamoto za wafanyabiashara.

III. **KUENDELEZA WELEDI WA WATUMISHI** wa ZRA kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini, na huduma nzuri kwa walipakodi (Customer care).

IV. **KUIMARISHA** upatikanaji wa taarifa za wageni wanaoingia Zanzibar kwa kuwasajili watoa huduma wote wanaotoa Huduma za Usafiri kwa Mtandao (Oline Traveling Agency-OTA), na kuimarisha usimamizi wa mfumo wa kutambua wageni wanaoingia Zanzibar wa GADIS.

V. **KUFANYA TAFITI** kwa lengo la kupata majibu ya Kisayansi yatakayoongeza urahisi wa kulipa Kodi kwa kuondoa **CHANGAMOTO** zinazojitokeza, na kuongeza wigo wa Kodi (Tax base).

VI. **KUONGEZA** idadi ya **WATUMISHI** wa Mamlaka kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma Kikodi kwa Walipakodi na Jamii kwa Ujumla.

VII. **KUONGEZA UBUNIFU** kwa Kurahisisha na Kuondoa usumbufu (Inconvinience) katika **KUIMARISHA HUDUMA** za Kodi (Elimu ya Kodi, Usajili wa kodi, Uwasilishaji wa Ritani, Malipo ya Kodi na Ukaguzi wa Kodi) katika ofisi za kodi za Mikoa na vituo vya huduma za kodi (Tax Service Centres), pamoja na kuimarisha Kituo cha Mawasiliano cha ZRA ili kurahisisha na kuimarisha ulipaji kodi wa hiari Zanzibar.

VIII. **KUIMARISHA** Kusomana (Interoperability) kwa Mfumo wa **ZIDRAS** na Mifumo ya taasisi nyingine zinazofanya kazi na ZRA ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi za Walipakodi.

IX. **KUWACHUKULIA HATUA** za Kisheria Walipakodi wachache wasiowajibika ipasavyo katika kutimiza wajibu wao wa kulipa Kodi.

4. **HITIMISHO**:

ZRA Inawashukuru Walipakodi wote kwa kulipa kodi kwa HIARI, na kuwaomba kuendelea kutoa Ushirikiano kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ili kuweza kukusanya mapato ya kodi, kwa wepesi na haki yatakayopelekea kutumika kuimarisha huduma bora za kijamii na maendeleo kwa wananchi wote.

**"Tulipe Kodi Kwa Maendeleo ya Zanzibar"**

CPA Yusuph Juma Mwenda
**KAMISHNA MKUU**